**SHULE YA SEKONDARI KWANGU**

**S.L.P 339**

**MWANGA**

**0719 529 734 / 0657 117 377**

**TAREHE___________________**

Jina la mwanafunzi________________________________________

**FOMU YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KWANGU, WILAYA YA MWANGA, MKOA WA KILIMANJARO MWAKA____________**

01. **UTANGULIZI**

Nina furaha kukuarifu kwamba umechaguliwa kuendelea na masomo au kujiunga na kidato cha kwanza shule ya sekondari **KWANGU**. Shule ipo umbali wa km **41** kaskazini mashariki kutoka makao makuu ya Halmashauri ya wilaya ya mwanga na umbali wa km **15** kutoka barabara kuu ya lami.

02**. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KWA WANAFUNZI WA KUTWA**

**(A)** Chakula cha wanafunzi wa kutwa ni muhimu sana na kinapatikana baada ya makubaliano ya wazazi wenyewe baada ya kufanya kikao kwa muhula wa kwanza kulingana na kalenda ya shule.

Matibabu kwa wanafunzi wa kutwa mzazi/mlezi unatakiwa kuhakikisha mwanao ana huduma ya Bima ya afya ya jamii ili kuepuka usumbufu wa matibabu, hatutapokea hela ya matibabu.

(B**) SARE YA SHULE KWA WAVULANA**

1. Mashati meupe mawili mikono mifupi yasiyobana.
2. Suruali mbili rangi ya **KIJIVU** (kwa kidato cha kwanza tu) yenye marinda mawili na isiyobana chini kipimo 18 **(MODO HAITAKIWI KABISA**).

   Kidato cha pili rangi ya suruali ni **UGORO** yenye vipimo sawa na maelekezo ya hapo juu.

   Kidato cha tatu na cha nne, rangi ya suruali ni **KIJANI (**chani kiwiti).
3. Tisheti ya rangi ya “**dark blue**” yenye kola (inapatikana katika duka la shule)
4. Sweta moja rangi inayoendana na rangi ya suruali yenye mshono wa (V) mbele.
5. Viatu vyeusi vya kufunga kamba na soksi rangi nyeusi.
6. Soksi nyeusi

**(C) WASICHANA**

1. Mashati mawili meupe mikono mifupi yasiyobana.
2. Sketi ya rangi ya **KIJIVU** ( kwa kidato cha kwanza tu) mshono wa rinda box inayovuka magoti mpaka kwenye jicho la mguu (ankle).

   Kidato cha pili rangi ya sketi ni **UGORO** na vipimo na mshono ni sawa kama ilivyoelekezwa hapo juu.

   Kidato cha tatu na cha nne, rangi ya sketi ni **KIJANI** (chani kiwiti) vipimo na mshono ni sawa na maelekezo ya hapo juu.
3. Rangi ya hijabu ifanane na sare ya shule (kwa wanafunzi waislamu tu)
4. Sweta moja rangi inayoendana na sketi yenye mshono wa (V) mbele.
5. Tshirt moja rangi ya "**dark blue**" yenye kola inapatikana katika duka la shule
6. Viatu vyeusi vya kamba visivyo na kisigino kirefu.
7. Soksi nyeupe pea mbili.

**2.1. SARE MUHIMU ZA MICHEZO**

1. Bukta moja nyekundu na fulana yake (kwa wasichana tu)
2. Bukta moja ya bluu na fulana yake (kwa wavulana tu)
3. Raba za michezo nyeupe (kwa wasichana tu) na rangi yoyote kwa wavulana.

**2.2. VIFAA VINGINE MUHIMU**

1. Daftari kubwa **12** kaunta, kalamu za kutosha, mkebe wa hesabu (vinapatikana duka la shule) kamusi ya Kiswahili moja, dictionary ya English to English moja.
2. Sahani na kijiko ni muhimu kwa ajili ya chakula cha mchana
3. Fagio moja wa chelewa, ndoo moja ndogo (mpya) kwa wanafunzi wa kutwa tu.
4. Jembe moja **JIPYA** lenye mpini (kwa wasichana tu)
5. Panga moja **JIPYA** (kwa wavulana tu)
6. Saa ya mkononi (kwa wanafunzi wote).

## 03. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu **No.25** ya mwaka **1978** na kama ilivyorekebishwa kwa sheria **No.10** ya mwaka **1995**. Aidha, shule inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na teknolojia yenye dhamana ya Elimu na Ofisi ya **RAIS – TAMISEMI** yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

1. Heshima kwa viongozi , wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

2. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.

3. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)

4. Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazopewa.

5. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.

6. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.

7. Kuvaa sare ya shule wakati unapotakiwa.

8. kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

9. Kutunza mali za umma.

### 3.1 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

1. Wizi
2. Uasherati na ushoga
3. Ubakaji
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kuberi na n.k
5. Kupigana au kupiga
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
7. Kudharau Bendera ya Taifa
8. Kuwa mjamzito/kupata mimba
9. Kuoa au kuolewa

10. Kutoa mimba
11. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
12. Kukataa adhabu kwa makusudi
13. Kuwa na simu ya mkononi shuleni au kutumia simu kinyume na utaratibu wa shule
14. Kutoroka au kwenda nje ya shule bila ruhusa

**4.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI**

1. Medical Examination Form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.

2. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai

3. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatayotolewa na shule.

**5.0 TAFADHALI SOMA KWA MAKINI MAELEZO/ MAAGIZO HAYA NA KUYATEKELEZA KIKAMIRIFU.**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI KWANGU**

____________________________________

**AUGUSTINO MANENTO MBAWA**

**MKUU WA SHULE**

**FOMU YA MZAZI/MLEZI KUKIRI AU KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI MASHARTI NA MAELEKEZO MENGINE MUHIMU YA SHULE**

| PICHA MZAZI/MLEZI | | PICHA MWANAFUNZI |
|---|---|---|

MIMI ___________________________AMBAYE NI MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI.

JINA LA MWANAFUNZI_______________________________KIDATO_________MWAKA____

NINAISHI MTAA WA____________________WILAYA_______________MKOA______

Ninakiri/kukubaliana na sheria, kanuni, masharti na maelekezo mengine muhimu kwa kuwa mwanangu amejiunga kusoma katika shule hii na endapo itatokea mwanangu atakiuka au kuvunja sheria, taratibu au kanuni za shule, basi sheria, taratibu na kanuni zichukue mkondo wake kwa aidha kumsimamisha masomo au kumfukuza kabisa shule.

Aidha, nakubaliana na sheria, taratibu, kanuni na maelekezo yote muhimu yaliyoelekezwa katika fomu hii ya kujiunga na shule kwa kuwa zinatokana na miongozo inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na teknolojia ambayo ndio yenye dhamana ya Elimu na pia ile inayotolewa na Ofisi ya **RAIS – TAMISEMI**, ofisi yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu hapa nchini chini ya kifungu cha sheria **No.25** ya mwaka **1978** na marekebisho yake chini ya sheria **No.10** ya mwaka **1995**.

**JINA LA MZAZI _______________________________**

**SAINI_______________________**

**TAREHE____________________**

**SHULE YA SEKONDARI KWANGU**

**FOMU YA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI**

**SEHEMU HII IJAZWE NA MWANAFUNZI MWENYEWE**

1. Jina kamili la mwanafunzi________________________________________

2. Tarehe ya kuzaliwa____________________________________

3. Kijiji/mtaa/wilaya
ulikozaliwa___________________________Mkoa_________________________

4. Dini/ dhehebu _______________________________________

5. Uraia_____________________________

6. Jina kamili la Baba/Mama/Mlezi_________________________________________

7. Namba ya simu ya Mzazi/Mlezi____________________________________________

8. Kijiji/Mtaa anapoishi mzazi/mlezi____________________________wilaya________

9. Kazi ya mzazi/Mlezi________________________________________

10. Kwa sasa unaishi na nani?
Mtaje___________________________________________

Una mahusiano gani na huyo uliyemtaja hapo juu______________________________

Anafanya kazi gani________________________

Je, anaishi kwenye nyumba ya kupanga? (NDIYO/HAPANA)

11. Ndugu wawili wa karibu (wanaweza kuwa mbadala wa wazazi)

(i) Jina_________________________________________

Una mahusiano gani naye________________________________

Mahusiano yake na mzazi________________________________

Namba yake ya simu____________________________________

(ii) Jina__________________________________________

Una mahusiano gani naye________________________________

Mahusiano yake na mzazi________________________________

Namba yake ya simu____________________________________

12. **AFYA**

(i) Je, ulishawahi kupatwa na magonjwa makubwa kama vile Tb, Kifafa,Polio N.K
(NDIYO/HAPANA)

(ii) Je, una upungufu wa matatizo yoyote ya viungo kama macho, kilema, n.k
(NDIYO/HAPANA)

13. TAJA JINA LA BALOZI WAKO_____________________________________

TAJA JINA LA AFISA MTENDAJI WA KATA YAKO_______________________

ANUANI/SIMU ________________________________

14. Tarehe_________________________________

___________________________

**AUGUSTINO MANENTO**

**MKUU WA SHULE**

**MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE AND TECHNOLOGY**

**KWANGU SECONDARY SCHOOL**

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

TO: Medical Officer

………………………………………………………

………………………………………………………

From: The Headmaster

Kwangu Secondary School

P.O.Box 339

MWANGA

Date…………………………………….

Students Name……………………………………………………………………………..

Please Examine the above named student as to his/her fitness for entrance to this school in form…………

i) Blood count (Red & White)……………………………………………………………………………………….

ii) Stool Examination…………………………………………………………………………………………………

iii) Urinal Analysis…………………………………………………………………………………………………….

iv) TB Test……………………………………………………………………………………………………………..

v) Syphilis Test………………………………………………………………………………………………………..

vi) Eye test……………………………………………………………………………………………………………

vii) Ears………………………………………………………………………………………………………………..

viii) Chest…………………………………………………………………………………………………………….

ix) Spleen…………………………………………………………………………………………………………….

x) Abdomen………………………………………………………………………………………………………….

(Check case of pregnancy in girls)

ADDDITIONAL Information (Eg. Physical Defects or Impairments, Infection, chronic or Family diseases Etc.)

…………………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………………

**MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by the Medical Officer)

I have examined the above names and consider that he/she is physically fit for appointment/re-engagement as above. He/she is not physically fit for appointment/engagement.

Date…………………………………………………………………. Signature…………………………………………….

Note to medical at the time of examination: Please treat any illness you not.

Delete as necessary.